Kiambatisho Cha II: Barua ya Human Rights Watch kwa Waziri wa Afya Ummy Mwalimu, Disemba 24, 2019

Mheshimiwa Ummy Mwalimu
Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto
Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto
Chuo Kikuu cha Dodoma,
Kitivo cha Sanaa na Sayansi ya Maendeleo ya Jamii,
Jengo No: 11,
S.L.P 573,
40478 Dodoma, Tanzania

Fax: +255 26 2963348
Barua pepe: ps@communitydevelopment.go.tz
Kupitia mtandao: imewasilishwa mtandaoni kupitia https://www.moh.go.tz/en/contact-us

Disemba 24, 2019

Mpendwa Mheshimiwa Waziri Ummy Mwalimu:

Tunakuandikia kwa niaba ya Human Rights Watch, shirika la kimataifa linalonukuu ukiukwaji wa haki za binaadamu katika nchi zaidi ya 100 ulimwenguni kote na kufanya kazi na serikali katika kuboresha usimamiaji wao wa haki za binadamu. Hivi karibuni, Human Rights Watch imenakili taarifa juu ya haki ya afya nchini Tanzania, hasa ikiangazia namna gani sheria na sera zimezuia makundi maalum, hasa wanaume wanaofanya mapenzi na wanaume wengine na watu wenye jinsia tofauti na asili, kunufaika na haki yao ya msingi ya kupata huduma bora ya afya iliyopo, kama inavyohakikishwa na sheria ya kimataifa. Hii ndio mada ya ripoti inayotarajiwa kutoka, na tungependa kuipatia ofisi yako fursa ya kupitia na kujibu matokeo ya utafiti wetu wa awali kufikia tarehe 10 Januari 2020, ili kwamba tujumuishe mtazamo wa serikali katika ripoti yetu itakayochapishwa.

Ripoti ni matokeo ya mahojiano na wanawake wanaofanya mapenzi na wanawake, wanaume wanaofanya mapenzi na wanaume, wanaovutiwa mapenzi na jinsia zote mbili na

watu wenye jinsia tofauti na asili(LGBT) wapatao 35 ambao wamekuwa wakiathirika moja kw amoja na sheria na sera ambazo ripoti inazichambua, pamoja na mashirika mengine ya Kitanzania, kikanda na kimataifa na wataalamu na wahisani wa masuala ya afya na haki za binaadamu na mashirika ya Umoja wa Kimataifa. Ripoti inatathmini matokeo ya sera kadhaa zinazotekelezwa na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, ikiwa ni pamoja na marufuku iliyowekwa katika vilainishi vya maji na silica, kuzuiwa kwa miradi ya elimu ya kujikinga na HIV inayoongozwa na mashirika ya asasi za kiraia zinazowawakilisha wanaume wanaofanya mapenzi na wanaume, na kufungwa kwa vituo vya afya vinavyotoa huduma za HIV kwa makundi maalum. Ripoti inanakili jinsi gani unyanyapaa na ubaguzi unaendelea kuathiri wanaume wanaofanya mapenzi na wanaume na watu wenye jinsia tofauti na asili katika vituo vya afya vya serikali, hali inayowazuia kupata huduma za afya. Inanakili pia matukio kadhaa ya uvamizi wa polisi katika warsha na mafunzo ya mashirika ya kiraia vikihusiana na afya na haki. Wakati tunafahamu juu ya jitihada za hivi karibuni za Wizara ya Afya kuboresha majadiliano na makundi maalum, kama vile uundwaji wa Kamati ya Ushauri ya Makundi Maalum, tunaendelea kusikitishwa sana kwamba Wizara ya Afya na mashirika mengine ya serikali bado yanaendelea kuweka vikwazo katika haki ya afya ya makundi maalum.

Upatikanaji wa Vilainishi Binafsi

Katazo la Wizara ya Afya la upatikanaji wa vilainishi binafsi linawaondolea watu kinga iliyothibitishwa dhidi ya maammbukizi ya HIV. Kwa mujibu wa taarifa ya wizara yako ya tarehe 27 Oktoba 2016, “Serikali na jamii ya Tanzania inahitaji kujiridhisha zaidi juu ya njia hii ikiwa inafaa na kukubalika nchini kabla ya kupigiwa chepuo kama njia madhubuti katika kuzuia HIV.”[303] Lakini hakuna shaka miongoni mwa mashirika ya afya ulimwenguni juu ya ufanisi wa kilainishi. Miongozo ya UNAIDS inasema “Programu zinapaswa kuvitoa vilainishi vya maji na silika pamoja na kondomu,” ikisema kwamba vilainishi ni vya muhimu sana kwa wanaume wanaofanya mapenzi na wanaume, wafanyabiashara wa ngono na wanawake wanaotarajia kujifungua.”[304] Hata Mkakati wa Pili wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI wa Tanzania ulitaka upatikanaji wa vilainishi, na Wizara ya Afya huko nyuma iliwahi kupigia chepuo upatikanaji wa vilainishi. Kuchagua kuzuia nyenzo muhimu

[303] Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, “Taarifa ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto. Mh. Ummy Mwalimu juu ya Huduma za HIV kwa Makundi Maalum nchini Tanzania, tarehe 27 Oktoba 2016.” Ipo katika faili la Human Rights Watch; inapatikana pia https://m.facebook.com/afyatz/posts/1230922863594845 (imepitiwa Mei 15, 2019).

[304] UNAIDS, Ujumbe wa Mwongozo, “Condom and lubricant programming in high HIV prevalence countries,” 2014, https://www.unaids.org/sites/default/files/media_asset/condoms_guidancenote_en.pdf (imepitiwa Juni 4, 2019).

ya kuzuia HIV kwa kisingizio cha “kukubalika” kijamii maana yake ni kuyaweka maisha ya watu hatarini kwa hiari.

Wengi wa wanaume wanaofanya mapenzi na wanaume na wanaume wanaovutiwa kimapenzi na jinsia zote mbili wapatao 23 waliohojiwa na Human Rights Watch walisema hawakuweza kupata vilainishi vya maji na vile vya silika pia. Baadhi ya waliohojiwa walisema hutumia mafuta ya nazi kama vilainishi, wakati wengine wakitumia mafuta ya kujipata mwilini kama vile Vaseline au yale ya watoto, ambayo yanaweza kuharibu kondomu. Wengine walisema wanatumia mate, ambayo hayatoi utelezi wa kutosha na yanaweza kusababisha kupasuka kwa kondomu, hali inayoongeza maambukizi ya HIV na magonjwa mengine ya zinaa.

Tungependa kupata majibu yako kwa maswali yafuatayo:

Ni hatua gani ambazo serikali imezichukua „kujiridhisha zaidi” kwamba vilainishi vya maji ni suluhisho mahususi la afya, kama ilivyosemwa katika taarifa ya wizara yako ya tarehe 27 Oktoba 2016?

Ni vigezo gani ambavyo wizara yako ilivitumia kutathmini “kukubaliwa nchini” kwa vilainishi vya maji kama suluhisho la kiafya, sababu iliyotajwa katika taarifa ya wizara yako ya Oktoba 27 2016?

Je, Wizara ya Afya ina mpango wa kuondoa katazo lake na kuruhusu uingizwaji na usambazwaji wa vilainishi, kama ambavyo ilivyopendekezwa mwaka 2015?

Uzuiwaji wa Huduma za HIV na Vituo vya Afya vya Makundi Maalum Vinavyoongozwa na Jamii

Utafiti wetu umegundua kwamba uzuiwaji wa “elimu kwa jamii ya wanaume wanaofanya mapenzi na wanaume na vituo vya msaada kwa wanaume wanaofanya mapenzi na wanaume” mwezi Oktoba 2016, baada ya maelekezo yako ya Februari 2017 kufunga vituo vyote vya msaada kwa makundi ya maalum na yaliyo katika hatari za kiafya, maana yake ni kwamba wanaume wengi wanaofanya mapenzi na wanaume, pamoja na makundi maalum mengine, hawataweza kupata kwa urahisi huduma za kinga ya HIV. Kama ambavyo mwanaume mmoja anayefanya mapenzi na wanaume alivyoiambia Human Rights Watch:

Kila nilipokuwa na tatizo la kiafya, niliweza kwenda kwenye kituo kupata msaada au kuunganishwa na mtoa huduma za afya ambaye hakuwa mbaguzi, ambaye alinihudumia kama watu wengine. Siku hizi, hata kama nina tatizo la kiafya, sina mahali pa kwenda ambapo naweza kulielezea tatizo langu, hivyo nanyamaza tu [na kuepuka kutafuta huduma].[305]

Tunafahamu kwamba serikali imeruhusu ufunguaji wa Vituo Mahiri vinavyoambatana na mradi wa Sauti katika majengo mbalimbali ya serikali, na kwamba baadhi ya wanaume wanaofanya mapenzi na wanaume wanaweza kwenda na kupatiwa huduma katika vituo hivi. Hata hivyo, mahojiano yetu yanaonyesha kwamba wengine wamekuta vituo hivyo vilivyopo kuwa vigumu kuingia au visivyokaribisha wageni ukilinganisha na vituo vya msaada ambavyo vilikuwa vikihudumia jamii hizi huko nyuma. Zaidi yah apo, wanaume wanaofanya mapenzi na wanaume pamoja na watu wasio na jinsia za asili hawapati tena huduma za mafunzo mbalimbali ambazo zilikuwa zikitolewa na mashirika ya kijamii. Wakati baadhi ya mashirika yanatoa mafunzo kwa wanaume wanaofanya mapenzi na wanaume, na kuwaajili wanaume wanaofanya mapenzi na wanaume kuwa waalimu kwa wenzao wenye urengwa kama wao, wahojiwa wengi walisema walipendelea mafunzo yaliyokuwa yakitolewa na mashirka ya kijamii yenyewe.

Kutokana na matokeo haya, tutashukuru kupata majibu yako juu ya maswali yafuatayo:

Wizara yako imefanya tathmini ya madhara ya kiafya ya katazo la Oktoba 2016 la "mafunzo ya jamii ya MSM na vituo vya msaada vya MSM" na agizo la Februari 2017 la kufunga vituo vyote vya msaada vya makundi maalum na yale yaliyohatarini?

Je serikali itaruhusu mashirika ya jamii kufungua tena vituo vya msaada na kufanya mafunzo juu ya uzuiaji wa VVU, kufuatana na utendaji bora wa kimataifa unaojulikana?

<u>Ukiukwaji wa Haki ya Kushirikiana (Kutengeneza Ushirika)</u>

Muongozo wa Taifa Jumuishi wa Kupabana na VVU kwa Makundi Maalum na Yaliyo katika Hatari wa Wizara ya Afya wa April 2017, umesema kwamba huduma rafiki kwa Makundi Maalum na Yaliyo Katika Hatari zinapaswa kujumuisha "msaada binafsi na ule wa

[305] Mahojiano kati ya Human Rights Watch na Medard (jina bandia), eneo limehifadhiwa, Mei 18, 2018.

kimakundi."[306] Hata hivyo, utafiti wetu umegundua kwamba makundi hayo kwa wanaume wanaofanya mapenzi na wanaume hayaruhusiwi kusajiliwa kama NGOs au kufanya kazi kwa usalama kwasababu yanashutumiwa "kutangaza mapenzi ya jinsia moja."

Mwezi Aprili 2019, Bodi ya Uratibu ya NGO, ambayo inafanya kazi chini yako, ilifutia ushajili wa mashirika sita, ikiwa ni pamoja na shirika liitwalo Community Health Education Services and Advocacy (CHESA), ambalo lilikuwa likitoa huduma za afya na kupigania haki za wana-LGBT.

Tutashukuru majibu yako kwa maswali yahusuyo hoja zifuatazo:

Ni hatua gani ambazo Wizara ya Afya inachukua kuwezesha uwepo na utendaji kazi wa misaada binafsi nay a kimakundi kwa MSM na watu wasio na jinsia ya asili, kufuatana na miongozo yenu yam waka 2017 na utendaji bora unaotambulika kimataifa?

Usajili wa CHESA ulifutwa kwa misingi gani?

Uamuzi huu unaendana vipi na wajibu wa Tanzania chini ya Mkataba wa Afrika wa haki za Watu na Binadamu na Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa kutekeleza haki ya kushirikiana (kutengeneza shirika) kwa wote, na utendaji bora wa kiataifa unaojulikana unaotaka kuwepo kwa kazi zinazoongozwa na jamii za kuzuia na kutibu VVU?

<u>Unyanyapaa katika Hospitali na Vituo vya Afya vya Serikali</u>

Miongozo ya Makundi Maalum na yale yaliyo Hatarini inasema pia kwamba "Wanaume wanaofanya mapenzia na wanaume na watu wasio na jinsia ya asili mara nyingi huwa hawahudumiwi vya kutosha na hawapati vifaa na fedha za kutosha….. jumla ya unyanyapaa, ubaguzi na ujinai unaozuia wanaume wanaofanya mapenzi na wanaume wengine na watu wasio na jinsia ya asili kupata huduma zilizopo. Kumekuwepo na kushindwa kwa dunia nzima katika kuelewa na kuchukua hatua za kutosha katika kuhudumia vya kutosha mahitaji yao ya kiafya na haki zao za bnadamu." Misingi Mikuu ya

[306] Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Programu ya Taifa ya Kupambana na UKIMWI, Aprili 2017, "National Guideline for Comprehensive Package of HIV Interventions for Key and Vulnerable Populations," https://hivpreventioncoalition.unaids.org/wp-content/uploads/2018/03/Tanzania-KP-GUIDELINE-1.pdf, p. 10.

Jumla katika miongozo hii ni pamoja na: “IBoresha mazingira ya sheria, sera na jamii kuwezesha makundi maalum nay ale yaliyopo hatarini kupata huduma za afya zilizopo.”[307]

Wengi wa wanaume wanaofanya mapenzi na wanaume na watu wasio na jinsia ya asili waliohojiwa na Human Rights Watch walisema wanakumbana na ubaguzi wanapokwenda kupata huduma za afya za serikali. Mwanaume anayevutiwa kimapenzi na mwanaume mwingine mwenye umri na miaka 24 na muathirika wa VVU alituambia kwamba muhudumu wa afya katika Hospitali ya Sinza Palestina, ambapo alikuwa anapata matibabu ya VVU, alimwambia: “Wewe ni kijana mzuri, kwanini unafanya mapenzi na wanaume wenzako? Ndio maana umepata UKIMWI, kwasababu hayo matendo yanamchukiza Mungu.” Muhojiwa huyo aliongeza “Waliniambia pia kwamba niache hii michezo na kuokoka, nimfukuze Shetani, anayenisababisha kufanya maoenzi na wanaume, na kupata mke, nioe na kuwa na familia.” Hatimaye aliipata NGO inayotoa huduma za afya rafiki kwa wana-LGBT, lakini kwa muda aliepuka kabisa kupata huduma za afya.[308]

Mwanaume mwingine anayevutiwa kimapenzi na mwanaume alituambia alipoenda Hospitali ya Mwananyamala Septemba 2018 kupima VVU, wahudumu wa afya pale “hawakufurahia nilipowaambia kwamba mimi ni mwanaume ninayevutiwa kimapenzi na mwanaume mwingine…. Walikuwa wanatumia lugha mbaya – ‘kama wewe ni mwanaume unayevutiwa kimapenzi na mwanaume mwingine, wakati mwingine usije tena katika hospitali hii, kwasababu hatutibu watu kama wewe.’”[309]

Tutashukuru kupata majibu yako juu ya matokeo haya:

Ni hatua gani ambazo Wizara ya Afya inachukua kuboresha mazingira ya kisheria, sera na jamii yanayowakabili wanaume wanaofanya mapenzi na wanaume na watu wasio na jinsia za asili nchini Tanzania ili kuboresha upatikanaji wa huduma?

---

[307] Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Programu ya Taifa ya Kupambana na UKIMWI, Aprili 2017, “National Guideline for Comprehensive Package of HIV Interventions for Key and Vulnerable Populations,” https://hivpreventioncoalition.unaids.org/wp-content/uploads/2018/03/Tanzania-KP-GUIDELINE-1.pdf, aya. 5, 8.

[308] Mahojiano kati ya Human Rights Watch interview na Osman (jina bandia), eneo limehifadhiwa, Mei 22, 2018.

[309] Mahojiano kwa njia ya simu kati ya Human Rights Watch na Suleiman (jina bandia), Oktoba 2, 2018.

Ni hatua gani hasa zilizochukuliwa kuhakikisha kwamba vituo vya afya vya serikali vinatoa huduma za afya kwa wanaume wanaofanya mapenzi na wanaume na watu wasio na jinsia asili bila ubaguzi?

Vipimo vya Nguvu vya Njia ya Haja Kubwa

Human Rights Watch iiliwahoji wanaume watatu nchini Tanzania ambao walifanyiwa vipimo vya nguvu vya njia ya haja kubwa. Kwa mujibu wa mjumbe maalum wa Umoja wa Mataifa anayeshughulikia mateso, "Katika nchi ambazo mapenzi ya jinsia moja ni kosa la jinai, wanaume wanaofanya mapenzi na wanaume wenzao wako hatarini kufanyiwa vipimo vya lazima vya sehemu ya njia kubwa vinavyolenga kupata Ushahidi wa kimwili wa mapenzi ya jinsia moja, kitendo ambacho hakina maana kitabibu na ni sawa na mateso."[310]

Ofisi ya Marekani ya Mratibu wa UKIMWI Duniani, ambayo inasimamia Mfuko wa Dharura wa Rais wa Marekani wa Kupambana na UKIMWI (PEPFAR), umeitaka Wizara ya Afya kutoa agizo likikataza vipimo vya nguvu vya njia ya haja kubwa katika utesaji wa watu walio katika mapenzi ya jinsia moja katika mazingira yoyote yale. Tunaelewa kwamba, badala ya kuweka katazo la mara moja, Wizara ya Afya alitengeneza Kamati ya Makundi Maalum na Yaliyo Hatarini, pakiwa na uwakilishi wa wanaume wanaofanya mapenzi na wanaume, na kwamba moja ya makusudi ya kamati hiyo ni kutengeneza waraka ambao utapiga marufuku upimwaji wa nguvu wa njia ya haja kubwa.

Tutashukuru kupata majibu yako kwa maswali yafuatayo:

Ni Muongozo gani ambao Wizara ya Afya iliutoa kwa watumishi wa afya juu ya vipimo vya nguvu vya njia ya haja kubwa kwa ajili ya mateso ya wapenzi wa jinsia moja?

Je wizara ya afya inapanga kuwakataza watumishi wa afya kufanya vipimo vya nguvu vya njia ya haja kubwa kwa ajili ya matesi ya wapenzi wa jinsia moja?

* * *

[310] Baraza la Haki za Binadamu la Umoja wa Mataifa, "Report of the Special Rapporteur on torture and other cruel, inhuman or degrading treatment or punishment," A/HRC/31/57, Januari 5, 2016, http://www.refworld.org/docid/56c435714.html (imepitiwa Mei 19, 2016), aya. 36.

Tutashukuru kupata majibu yako katika maswali haya na taarifa zingine za ziada juu ya jitihada za serikali katika kuzuia VVU na sera zake zingine za afya kuhusiana na makundi maalum kufikia Januari 13, 2020. Ikiwa tarehe hiyo itapita, tutashindwa kuyajumuisha majibu yenu katika ripoti yetu itakayotoka. Tafadhari tuma majibu kwa mtafiti wetu mwandamizi, Bi. Neela Ghoshal, kupitia [redacted]

Tunasubiria kwa hamu mahojiano mazuri katika kupigania haki ya upatikanaji wa huduma bora zaidi za afya kwa Watanzania wote, bila kujali urengwa wao wa kingono au utambulisho wa kijinsia.

Wako Mwaminifu,

Graeme Reid
Mkurugenzi, Programu ya Haki za LGBT

Mausi Segun
Mkurugenzi Mtendaji, Idara ya Afrika ya Human Rights Watch